



**KISII UNIVERSITY**  
**UNIVERSITY EXAMINATIONS**  
**SPECIAL/SUPPLEMENTARY EXAMINATIONS**  
SECOND YEAR EXAMINATION FOR THE AWARD OF  
THE DEGREE OF BACHELORS OF ARTS / EDUCATION  
SECOND SEMESTER 2024/2025  
(AUGUST, 2025)

**KISW 225: USHAIRI WA KISASA (MODERN SWAHILI POETRY)**

**STREAM: Y2 S2**

**TIME: 2 HOURS**

**DAY: TUESDAY, 9.00 – 11.00 A M**  
**05/08/2025**

**DATE:**

---

**MAAGIZO**

1. **Usiandike neno lolote kwenye karatasi ya maswali.**
2. **Jibu Maswali MATATU. Swali La Kwanza na mengine Mawili.**

1. a) Fafanua ubishi na migogoro iliyoko baina ya makundi ya Ushairi wa kimapokeo na kundi la Ushairi wa sasa la kimabadiliko au kimapinduzi.

(alama 10)

b) Tambua aina tano za ushairi na kueleza sifa nne kwa kila moja ya ushairi ulioutambua ukirejelea mifano yoyote mwafaka.

(alama 20)

2. Ukirejelea vipindi mbalimbali vya ukuaji wa Ushairi kwa jumla, eleza matapo mbalimbali ya ushairi wa Kiswahili.

(alama 20)

3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata:

- 1 Hae! Msiba mzito, amefishwa Shaabani,  
*Nyoyo zinawaka moto, imetujaa huzuni,*  
 Lughu yetu bado toto, mlezi sasa ni nani?  
 Kafariki Shaabani, mlezi wa Kiswahili.
2. Kwa kulea Kiswahili, shekhe wetu Shaabani,  
 Safu yake ya awali, kwa tungo zenye thamani,

*Mahiri* mwenye akili, kwa tenzi hana kifani,  
Ole kafa Shaabani, mlezi wa Kiswahili.

3. Atokezapo kuranda, kwa nia ya ushindani,  
Hazuki wa kumshinda, kwa rai zenye uzani,  
Kila hoja huipanda, akatawala medani,  
Hae! Kafa Shaabani, mlezi wa Kiswahili.
4. Kwa lugha hana mwenziwe, kwa ujuzi wa undani,  
Kama yupo nitajiwe, ni nani huyo ni nani,  
Atoke atunukiwe, *avikwe koa shingoni*,  
Apambwe kama Shaabani, mlezi wa Kiswahili
5. Hasara thama hasara, kufariki Shaabani,  
Imezimika Zuhura, nyota yetu maangani,  
Laiti iwe kafara, lugha ikuzwe nchini,  
Kwa kifo cha Shaabani, mlezi wa Kiswahili.
6. Bure ustaarabu, usio usio na tamaduni,  
Mfano wa mke bubu, hafurahishi nyumbani,  
Akifa mtu adibu, lugha huwa makiwani,  
Kama kufa Shaabani, mlezi wa Kiswahili.

a) Fafanua muundo wa shairi ulilolisoma. (alama 6)

b) Tambua na kueleza mbinu za matumizi ya lugha alizozitumia mtunzi.

(alama 4)

c) Hakiki maudhui katika ushairi uliuousoma hapa juu. (alama 6)

d) Eleza jinsi mtunzi wa shairi alivyoutumia uhurubwake wa kishairi.

(alama 4)

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Kuzimu wenda kuona, kila mdharau chake,  
Cha kwake akakikana, *kutumai* cha mwenzake,  
Fahamu amayo *lana*, mpiga chake mateke,  
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.

Siringe na kujivuna, chako ukakipa teke

Unavunja lako jina, ili watu wakucheke,  
Ana lana kwa Rabana, kila mdharau chake,

Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Chako japo si cha mana, kibaya mtu ni chake,  
Unavunja lako jina, ili watu wakucheke,  
Ana lana kwa Rabana, kila mdharau chake,  
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.

Awe Fatu na Amina, au Asha ndugu yake

Katu hawatafanana, kila mtu hadhi yake,

Kila mjuzi wa mana, huwa hadharau chake

Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Tama naomba amina, kilicho chetu tushikr

Kidumu na kulingana, na tukipe hadhi yake,

Ana lana kwa Rabana, kila mdharau chake

Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.

- a) Eleza muundo wa shairi ulilolisoma hapa juu. (alama 6)
- b) Andika beti mbili za kwanza za shairi hili kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- c) Ukirejelea mifano mwafaka, eleza jinsi mwandishi wa shairi hili alivyotumia uhuru wake wa utunzi. (alama 4)
- d) Jadili maudhui katika shairi hili. (alama 6)